# UTANGULIZI

- Zao linachangia mapato ya kigeni kwa wastani wa Dola 45 milioni kwa mwaka.
- Zao hili linatoa ajira kwa zaidi ya watu milioni 2,
  - (Ajira za viwandani na mashambani - takribani watu 50,000, na ajira zisizo za moja kwa moja - takribani watu 2,000,000).
  - Wakulima Wadogo wanakadiriwa kuwa takriban 32,000. Bodi inaendelea na zoezi la kuhakiki idadi ya wakulima wote wa chai kwa kuwasajili katika mfumo wa kielektoniki.
- Zao la chai linatekeleza kwa vitendo azma ya Serikali ya awamu ya sita ya kuzalisha chai kibiashara na kuliingizia taifa mapato ya kigeni kwa kuuza katika masoko ya nje (Agenda 10/30).

# Muundo wa tasnia ya chai Tanzania

- **Taasisi za Serikali:** zimeundwa kwa Sheria ya Chai namba 3 ya mwaka 1997 na marekebisho yake ya mwaka 2009;
  - Bodi ya Chai Tanzania (TBT) - jukumu la kusimamia Tasnia ya Chai (regulatory functions)
  - Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (TSHTDA) – jukumu la kuendeleza zao kupitia Wakulima wadogo wa chai
  - Taasisi ya Utafiti wa zao la Chai Tanzania (TRIT) –jukumu la kufanya utafiti wa zao la chai hapa nchini.
  - **NB: Mgawanyo huu upo kwenye nchi zote zinazolima chai**
- **Taasisi binafsi**
  - Umoja wa Wakulima Wakubwa wa Chai Tanzania (TAT) – kuwaunganisha wenye mashamba makubwa na wamiliki wa viwanda
  - Vyama vya Ushirika wa Wakulima Wadogo wa Chai (AMCOS). Kwa sasa zipo AMCOS 50 za wakulima wadogo na vyama vya upili (JE) vinne (4)

## 1.2 Shughuli za kiutendaji katika tasnia ya chai

Shughuli za kiutendaji zimegawanyika katika sehemu kuu tatu:

- **Uzalishaji wa majani mabichi ya chai** - Hufanywa na Wakulima Wakubwa na Wadogo.
- **Usindikaji wa majani mabichi ya chai** - Kuna viwanda 24 vya kusindika majani mabichi ya chai nchini, kati ya hivyo 19 ndio vinafanya kazi.
- **Uchanganyaji na ufungashaji kwenye vikasha** – Kuna viwanda 15 vinavyofanya kazi ya kuchanganya na kufunga kwenye vikasha. Kati ya hivyo 10 ndio vinafanya kazi.

# MAJUKUMU YA TAASISI ZINAZOTOA HUDUMA

## Bodi ya Chai Tanzania

- Majukumu ya Bodi ya Chai kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Chai yamegawanyika katika maeneo yafuatayo:
  - Kuishauri Serikali juu ya sera na mikakati ya kuendeleza Tasnia ya chai nchini;
  - Kuhamasisha na kusimamia uzalishaji, usindikaji, uhifadhi wa chai pamoja na bidhaa zitokanazo na chai;
  - Kuhamasisha na kusimamia masoko ya chai ndani na nje ya nchi (leseni, vibali na kutafuta masoko)
  - Kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa na takwimu za chai;

# MAJUKUMU YA TAASISI ......

**Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania**

- Majukumu ya TSHTDA kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Chai Nambari 3 ya mwaka 1997 ni kama ifuatavyo:
  - Kujenga na kukuza uwezo wa wakulima wadogo wa chai;
  - Kuwezesha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wadogo wa chai;
  - Kujenga na kuimarisha umoja wa Wakulima Wadogo wa Chai kupitia vikundi na vyama vyao;
  - Kuwezesha uendelezaji wa kilimo cha chai katika maeneo mapya; na
  - Kuwahamasisha wakulima wadogo wa chai kujenga na kuendesha viwanda vyao vya kusindika majani mabichi ya chai.

# MAJUKUMU YA TAASISI ......

**Taasisi ya Utafiti wa Chai**

- Kufanyia utafiti matatizo yote yanayohusiana na Chai, ikihusisha Uzalishaji, Utengenezaji, Ubora, Mfumo wa kilimo inayohusisha na mazao mengine na pamoja kazi za uuzaji/masoko
- Kukuza na kutekeleza program za kitafiti zinazolenga kutatua matatizo yaliyotambuliwa yanahusiana na Uzalishaji, Utengenezaji, Ubora, Mfumo wa kilimo na mambo mengine yanayohusiana na usimmamizi wa mazao.
- Kuongeza matokeo ya Utafiti wa tasnia ya Chai na kutanua jamii ya kisayansi katika njia sahihi kupitia machapisho, ripoti za kisayansi, Ziara mashambani, makongamano, mikutano, Semina na mafunzo ya muda mfupi.
- Kuanzisha na kudumisha ukusanyaji wa nyenzo, maandiko na data zote za kisayansi zina zohusiana na shughuli za kitafiti
- Kukuza, Kusaidia na kushauri njia zote zinazoathiri utafiti wa chai, mafunzo na ugani, maendeleo, na kuiwakilisha Serikali katika shughuli za kitafiti.

# DIRA NA DHIMA

- ***Dira:***
  - Kujenga hali ya utulivu na kuleta mafanikio katika kuendeleza ukuaji wa Tasnia ya Chai nchini**.**
- ***Dhima:***
  - Kusimamia kuendeleza na kudhibiti masuala yote yahusuyo Tasnia ya chai nchini kwa ufanisi, uhakika na usawa.

# USIMAMIZI NA MUUNDO WA UTENDAJI KAZI WA TAASISI

**Bodi za Wakurugenzi**

- Bodi za Wakurugenzi za Taasisi za Umma katika Tasnia ya Chai zinaundwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Chai. Jukumu kuu la Bodi hizi ni kushauri na kuongoza utekelezaji wa majukumu ya Taasisi yanayolenga kuendeleza Tasnia ya Chai.

**Usimamizi wa Taasisi**

- Shughuli za usimamizi na utendaji wa Taasisi zinafanywa na menejimenti zilizoundwa kwa kufuata miundo iliyoidhinishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pamoja na muundo wa kiutumishi, Taasisi hizi zinatekeleza majukumu kwa mujibu wa miongozo na waraka mbalimbali zinazotolewa na Wizara za kisekta.

**Taasisi hizi zina ofisi za kanda kama ifuatavyo:**

- **Kanda ya Nyanda za juu Kusini**, (Wilaya ya Rungwe, Njombe, Mufindi, Ludewa, Wanging'ombe na Kilolo);
- **Kanda ya Kaskazini**, (Wilaya ya Lushoto, Korogwe na Muheza);
- Kwa upande wa Mkoa wa Kagera na Mara usimamizi wa zao unafanyika kupitia makao makuu na pia kwa kushirikiana na wataalam wa kilimo waliopo katika ofisi za halmashauri za wilaya (Bukoba, Muleba na Tarime).

# MAPATO YA BODI YA CHAI, WAKALA WA CHAI NA TAASISI YA UTAFITI WA CHAI

- Mapato ya Bodi ya Chai Tanzania

| Na | Chanzo cha Mapato | | Mapato Halisi | | Bajeti iliyopitishwa | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | TSHS | 2020/2021 | 2021/2022 | | |
| 1 | Ruzuku ya Serikali | Matumizi Kawaida (Other Charges) | 101,052,160 | 93,473,348 | | |
| | | Mishahara (PE) | 419,310,479 | 297,988,366 | | |
| | | Maendeleo (Dev) | - | 219,920,000 | | |
| 3 | Mengineyo (Own Source) | Pango (Rent) &Other income | 163,185,466 | 157,959,595 | | |
| | | Wadau (Stakeholders) | 30,773,873 | 21,662,247 | | |
| | JUMLA | | 714,321,978 | 791,003,556 | | |

# MAPATO YA BODI YA CHAI, WAKALA WA CHAI NA TAASISI YA UTAFITI WA CHAI..........

- Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzaia

| Chanzo cha Mapato | Mapato Halisi | | Bajeti iliyopitishwa | |
|---|---|---|---|---|
| | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 | 2023/2024 |
| **Fedha za matumizi mengine (OC)** | 78,660,000 | 78,660,000 | 178,660,000 | 500,000,000 |
| **Fedha za Mishahara (PE)** | 600,967,293 | 749,099,158 | 792,551,700 | 750,029,383 |
| **Fedha za Maendeleo (Ndani)** | 0 | 115,000,000 | 300,000,000 | 500,000,000 |
| **Fedha za Maendeleo (Nje)** | | 370,000,000 | 370,000,000 | 370,000,000 |
| **Mapato ya ndani** | 450,000,000 | 200,000,000 | 350,000,000 | 400,000,000 |
| **Jumla** | 1,129,627,293 | 1,512,759,158 | 1,991,211,700 | 2,520,029,383 |

# MAPATO YA BODI YA CHAI, WAKALA WA CHAI NA TAASISI YA UTAFITI WA CHAI……….

- Taasisi ya Utafiti

| CHANZO CHA FEDHA | MAPATO HALISI | | BAJETI ILIYOPITISHWA | |
|---|---|---|---|---|
| | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 | 2023/2024 |
| Agri CONNECT Project | 228,200,000 | 490,150,462 | 541,666,482 | 285,404,453 |
| Ruzuku ya serikali (Government Contributions (DEV)) | 0 | 300,000,000 | 500,000,000 | 500,000,000 |
| Ruzuku ya serikali (Government Contributions (PE)) | 324,902,700 | 407,948,469 | 471,035,753 | 784,532,000 |
| Ruzuku ya serikali (Government Contributions (OC)) | 19,791,374 | 19,791,374 | 119,791,374 | 219,661,000 |
| OWN SOURCE | 513,530,054 | 315,430,844 | 483,723,668 | 450,000,000 |
| TOTAL | 858,452,328.00 | 1,533,321,149.11 | 2,116,217,276.74 | 2,239,597,452.84 |

# PROGRAMU NA MIRADI MBALIMBALI INAYOTEKELEZWA KATIKA TASNIA YA CHAI

**Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II)**

Kati ya maeneo ya utekelezaji wa ASDP II ambayo Tasnia ya chai itajikita zaidi ni pamoja na:

i. Usimamizi endelevu wa matumizi ya Ardhi

ii. Kuongeza tija na faida katika kilimo kwa kuhamasisha kutumia vipando bora pamoja na tafiti zinazofanya na TRIT kuhusiana na mifumo bora ya umwagiliaji na mashine rahisi za kuvunia.

**Miradi iliyopo ndani ya tasnia katika Wilaya ya Mufindi na Njombe:**

**Wilaya ya Njombe – Chai Project**

Mradi unatekelezwa kwa ufadhili wa Taasisi ya The Wood Foundation Africa

Wanashirikiana na wakulima wadogo kupitia Ushirika wa Wakulima wa

Mradi umelenga kupanua maeneo ya Wakulima Wadogo hadi kufikia hekta 2,500 ifikapo mwaka 2024/2025.

Mpaka sasa Wakulima Wadogo kupitia kampuni ya kutoa huduma kwa wakulima wadogo (Njombe Outgrowers Service Company-NOSC) wameshapanda zaidi ya hekta 2,300.

# PROGRAMU NA MIRADI MBALIMBALI INAYOTEKELEZWA KATIKA TASNIA YA CHAI.........

**Mradi wa EU- Agriconnect**

- Mradi huu unafadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya na unanufaisha wakulima wadogo wa chai katika Wilaya ya Mufindi, Njombe na Rungwe.
- Mradi unatekeleza na taasisi zifuatazo TSHTDA, TRIT, IDH, SOLIDARIDAD na CEFA.
- Shughuli za mradi; uzalishaji wa miche ya chai, ukarabati wa barabara, lishe na kuratibu mkutano wa wadau, marekebisho ya sheria na maandalizi ya uanzishwaji wa soko la chai hapa nchini.

**Mradi wa Her Money Her Life (Kazi Yetu na Care International)**

- Mradi huu unafadhiliwa na Care International ambapo unalenga kuwajengea uwezo Wakulima wadogo wa chai
- kuongeza uzalishaji na kushiriki katika mnyororo wa thamani wa zao kwa kufanya usindikaji.
- Mradi una mpango wa kuwawezesha Wakulima wa Korogwe chini ya chama cha ushirika Sakare chini ya makubaliano maalumu. Bodi ya Chai na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai tumejipanga kuhakikiasha makubaliano haya yanakuwa na matokeo chanya.

# MAFANIKIO

## 1. Uanzishwaji wa Mnada wa Chai wa Dar es salaam (DTA)

- kuendeshea mnada upo tayari ambapo Taasisi ya TMX ndio itasimamia shughuli hii.
- Kanuni za soko na mwongozo zimekwisha andaliwa
- Usajili wa ghala na maabara ya kuonjea chai umefanyika
- Usajili wa Wanunuzi na Mawakala (Brokers) unaendelea
- Majaribio ya soko yanaendelea kufanyika ili wadau wote muhimu waweze kushiriki kwa ufanisi

## 2. Kusimamia utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya tasnia ya chai.

- Bodi ya chai Tanzania kwa kushirikiana na wadau imekua kiongozi katika kutekeleza mikakati mbalimbli ya Tasnia ya chai.
- Mkakati wa mwaka 2012/13 – 2022/23 ulilenga kufikia uzalishaji wa chai kavu kwa tani 50,000.
- Kwa sasa wadau wa tasnia wameanza maandalizi ya mkakati mwingine ili kuendana na mabadiliko ya kisera na biashara ya chai.
- Kukamilika kwa mkakati wa Tasnia kutawezesha Taasisi na wadau kuandaa mikakati mahsus ya kitaasisi.

# MAFANIKIO.......

## 3. Utoaji wa Huduma za Ugani.

- Shughuli ya utoaji wa huduma za ugani mahsusi kwa wakulima wadogo wa zao la chai zinafanywa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania.
- Kutokana na changamoto ya uchache wa wafanyakazi, Wakala wa maendeleo ya wakulima Wadogo wa Chai Tanzania wanatoa huduma za ugani kwa kushirikiana na baadhi ya makampuni ya usindikaji na vyama vya ushirika katika mfumo wa PPP.
- Hii ni pamoja na kushirikiana na wadau wa maendeleo wanaofanya shughuli za kuendeleza wakulima wa chai.
- Wakala imesaini Randama ya Maelewano (MOU) na Mufindi Out Grower Project (MOG), Njombe Out growers Service Company (NOSC), na Chama cha upili cha Wakulima wa Chai wa Rungwe na Busokelo (RUBUTCOJE) na kutoa maafisa Ugani.
- Lengo kuu ni kuchangia gharama za uwezeshaji na kuweka malengo kwa maafisa ugani. Katika makubaliano hayo Serikali inachangia Mshahara  na makampuni yanatoa vitendea kazi, pesa ya kujikimu, mafuta ya pikipiki na mawasiliano.

# MAFANIKIO.......

## 4. Shughuli za Utafiti

- Umwagiliaji na matumizi ya maji katika uzalishaji wa zao la chai;
- Uboreshaji wa Aina ya Miche katika zao la chai ambapo aina mpya nane za miche iliyotolewa inaendelea kusambazwa kulingana na ufanisi wa michai katika eneo husika.
- Rutuba ya Udongo na matumizi ya mbolea: Tafiti mbalimbali kuhusiana na aina ya mbolea na rutuba za udongo zinaendelea ikiwemo kutoa mapendekezo ya aina za mbolea zinazotakiwa kutumika
- Uhaulishaji na Usambazaji wa teknolojia mpya kwa Wakulima wa zao la chai. Tafiti za technologia/mashine rahisi za kuvunia chai zinaendelea ili kurahisisha na kupunguza gharama za uzalishaji.

# MAFANIKIO.......

5. Kuhamasisha upanuzi wa mashamba/kilimo cha chai

- Zao la chai kwa sasa linalimwa katika Wilaya 12 ambazo ni Rungwe-Mbeya, Njombe, Wanging'ombe na Ludewa-Njombe, Mufindi na Kilolo-Iringa, Lushoto, Korogwe na Muheza-Tanga, Bukoba, na Muleba-Kagera na Tarime-Mara.
- Kati ya wilaya hizo, wilaya ya Njombe ndiyo inayoongoza katika upanuzi wa mashamba. Hii ni kutokana na ufadhili wa kutoka kwa mbia wa maendeleo pamoja na kuwa na mfumo mzuri wa utoaji wa elimu kwa wakulima kupitia TSHTDA na kampuni ya NOSC.
- Katika kipindi cha miaka mitano wakulima walio chini ya usimamizi wa NOSC wameweza kupanda jumla ya hekta 2,300. Jedwali lifuatalo linaonesha ukuaji wa maeneo ya chai kisekta

# MAFANIKIO…….

## Ukuaji wa maeneo yaliyopandwa chai kisekta

| Mwaka | Wakulima wakubwa (ha) | Wakulima wadogo (ha) | Jumla |
|---|---|---|---|
| 1961/62 | 7,797 | 60 | 7,857 |
| 1972/73 | 9,248 | 5,878 | 15,165 |
| 1980/81 | 9,258 | 10,234 | 19,492 |
| 1990/91 | 10,173 | 10,654 | 20,827 |
| 2000/01 | 10,628 | 10,668 | 21,296 |
| 2017/2018 | 11,272.1 | 11,449.45 | 22,721.55 |
| Hivi sasa | 12,207.10 | 11,598.45 | 23,805.55 |

# MAFANIKIO.......


**6. Uanzishwaji wa Mfumo wa kusajili na kutunza taarifa za Wadau wa Chai**

- Maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa utunzaji wa taarifa na takwimu muhimu za wazalishaji na uzalishaji wa chai na taarifa za masoko umekamilika.
- Mfumo huu utawezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za wazalishaji zitakazotumika katika kuweka mipango na mikakati ya kuendeleza zao ikiwemo kujua mahitaji ya pembejeo na miche bora ya chai.
- Shughuli ya ukusanyaji wa taarifa na usajili wa wakulima imeanza.

**7. Kusimamia uzalishaji;**

- Shughuli za udhibiti wa zao ili kufikia viwango vya ubora unaokidhi mahitaji ya soko zinafanywa na wataalam wa Bodi ya Chai Tanzania.

# UZALISHAJI WA CHAI KAVU (Kgs)





| | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Wakulima Wakubwa | 21,650,619 | 23,447,952 | 16,895,021 | 16,030,597 | 14,020,868 |
| Wakulima Wadogo | 12,360,034 | 13,744,651 | 11,819,651 | 11,478,841 | 10,803,759 |
| Jumla | 34,010,653 | 37,192,604 | 28,714,672 | 27,509,438 | 24,824,627 |

# MAFANIKIO.......

## 7. Kusimamia masoko

Zaidi ya asilimia 80 ya chai kavu inayozalishwa hapa nchini huuzwa kwenye masoko ya nje ya nchi na kiasi kilichobakia cha asilimia 20 huuzwa katika soko la ndani (nchini).


**Mauzo ya chai kavu nje ya nchi**




| | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo (Kg) | 29,160,642 | 28,874,981 | 23,187,274 | 24,077,040 | 23,201,534 |
| Mapato (US$) | 62,167,167 | 43,239,975 | 34,248,304 | 39,011,476 | 34,588,820 |
| Wastani wa Bei (US$/Kg) | 2.13 | 1.50 | 1.48 | 1.62 | 1.49 |

# MAFANIKIO…….

**Mauzo ya chai Kavu ndani ya nchi (Local sales)**




| | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo (Kg) | 5,434,406 | 3,926,817 | 3,767,989 | 3,722,059 | 3,161,573 |
| Mapato (US$) | 3,294,458 | 3,155,352 | 3,052,826 | 3,180,111 | 2,446,038 |
| Wastani wa Bei (US$/Kg) | 6,062 | 8,035 | 8,102 | 8,544 | 7,737 |

# MAFANIKIO .......

**9. Kuhamasisha uundwaji wa Vyama vya Ushirika**

Kufuatia agizo la Serikali kwamba, mazao yote ya kimkakati yauzwe kupitia vyama vya ushirika, Taasisi zinazosimamia zao kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika tunashirikiana katika kuhamasisha uundwaji wa vyama vya ushirika. Hii ni pamoja na kufanikisha uundwaji wa vyama vya msingi (50), vyama vya upili (2) na chama kilele.

**10. Kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya pamoja**

Bodi ya chai inaendelea na usimamizi wa shughuli za pamoja ikiwemo utoaji wa huduma za ugani, uzalishaji wa miche bora ya chai, shughuli za kitafiti na masuala ya masoko ya chai ikiwemo uanzishwaji wa mnada wa chai hapa nchini.

# CHANGAMOTO

**Changamoto za Kitaasisi (Bodi ya Chai Tanzania, Wakala wa Chai na Taasisi ya Utafiti)**

- Ufinyu wa bajeti hivyo kushindwa kutekeleza majukumu ya Taasisi kikamilifI
- Upungufu wa watumishi kwenye ofisi kuu na ofisi za kanda na maeneo yanayolima chai;
- Mishahara duni inayosababisha baadhi ya watumishi kuacha kazi na kutafuta kwenye mashirika ambayo viwango vya mishahara vipo juu. Ukilinganisha na Bodi nyingine za mazao, kiwango cha mishahara katika Taasisi tajwa viko chini.
- Uchache na uduni wa vitendea kazi kwa ajili ya kuwafikia wadau kwa wakati na kutoa huduma kwa ufanisi.

# CHANGAMOTO

**Changamoto za Uendelezaji wa Tasnia ya Chai Tanzania**

- Tija ndogo ya uzalishaji wa chai (wakulima wadogo wa chai ambayo ni kilo 1,000 kwa hekta, Wakulima wakubwa wastani wa kilo 1,500) wakati fursa ni kuzalisha zaidi ya kilo 2,500 kwa hekta kwa mwaka.
- Hali duni ya miundombinu (Barabara) kwenye maeneo yanayolima chai. Ubovu wa barabara katika maeneo yanayolima chai unaathiri usafirishaji wa majani mabichi ya chai kutoka kwa wakulima wadogo kwenda viwandani na chai kavu kutoka viwandani kwenda sokoni. Kwa wastani wa zaidi ya tani 5 za chai hupotea kutokana na miundombinu ya barabara kutopitika hasa kipindi cha masika ambacho uzalishaji wa chai unakuwa juu (peak season).
- Mabadiliko ya tabia nchi yameathiri uzalishaji kwenye maeneo mengi yanayolima zao la chai hapa nchini. Kiwango cha siku za mvua kimepungua kutoka siku 120 kwa mwaka hadi chini ya siku 90 na kusababisha kuwa na kipindi kirefu cha kiangazi ambacho kimeathiri uzalishaji wa chai kwenye maeneo yanayolima chai.

# CHANGAMOTO

**Changamoto za Uendelezaji wa Tasnia ya Chai Tanzania**

- Ukosefu wa kiwanda cha kusindika majani mabichi ya chai katika Wilaya ya Kilolo hali inayopelekea zaidi ya hekta 200 kutelekezwa na kutokuvunwa. Pia baadhi ya Wakulima wametekeza mashamba yao kutokana na changamoto mbalimbali.
- Mashamba ya chai – Kilolo Mashamba ya chai - Bumbuli-Lushoto
- Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye bei ya chai inayouzwa kwenye soko la ndani;
- Utegemezi wa soko la nje katika mauzo ya chai kavu. Suala hili linachangia kushuka kwa uzalishaji pindi kunapokuwa na changamoto za kimasoko kama ambavyo Tasnia imekubwa katika kipindi cha miaka mitatu baada ya kuibuka kwa ugonjwa wa UVIKO 19 na kuanza kwa vita kati ya Ukreini na Urusi.

# MIKAKATI YA TASNIA

**Mikakati ya kuongeza uzalishaji wa zao la chai**

- Kupanua kilimo cha chai kwenye maeneo mapya. Upanuzi mkubwa wa kilimo cha chai katika Wilaya ya Njombe na Mufindi unaendelea kufanyika. Kwa Upande wa Wilaya ya Njombe eneo jipya la hekta 2,300 zimeshapandwa chai na wakulima wadogo kupitia mradi wa Wood Foundation Africa kuanzia mwaka 2019/2020 kati ya lengo la kupanda hekta 2,500.
- Katika Wilaya ya Kilolo kuna ardhi yenye ukubwa wa hekta 3,600 ambayo yametengwa kwa ajili ya mashamba makubwa ya chai na 3,000 kwa ajili ya mashamba ya wakulima wadogo. Mkakati uliopo kuhamasisha Wakulima na wawekezaji kulima chai katika mfumo wa mashamba ya pamoja (Block farms).

# MIKAKATI YA TASNIA

- Kufufua mashamba yaliyotelekezwa kwa kusafisha, kupogoa, kujazia mapengo na kuweka mbolea. Kwa sasa jitihada zimeanza kufanyika za kufufua mashamba ya chai yaliyopo katika eneo la Dabaga, Wilaya ya Kilolo. Aidha wawekezaji wanaomiliki mashamba makubwa ya chai wameelekezwa kufufua mashamba ya chai yaliyotelekezwa.
- Kuendelea na uzalishaji wa miche bora ya chai kwa ajili ya kupanua maeneo mapya na kujazia mapengo. Shughuli hii inafanywa kwa ushirikishwaji wa Taasisi za umma, Sekta binafsi na wadau wa Maendeleo.
- Kuimarisha utafiti katika zao la chai ili kuzalisha miche bora ya chai yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi.

# MAEENEO YA KIPAUMBELE

**Maeneo ya kipaumbele kwa taasisi**

- Kuboresha mapato ya taasisi: Mkakati uliopo ni kuwa na chanzo endelevu cha mapato ya Taasisi ikiwemo kuanza kutoza ushuru wa huduma zinazotolewa na Bodi.
- Kuongeza idadi ya watumishi; Hii ni pamoja na kufanya mapitio ya muundo wa utumishi ili kuborehsa maslahi ya watumishi.
- Kuimarisha vitendea kazi yakiwemo magari na pikipiki; Suala hili linafanyiwa kazi kupitia bajeti za Taasisi
- Kuendelea kusimamia na kuimarisha mfumo wa upangaji bei ya majani mabichi ya chai kwa wakulima wadogo.

# MAENEO YA KIPAUMBELE

**Tasnia ya Chai:**

- Kutafuta suluhu ya uendeshaji wa makampuni ya chai yasiyofanya vizuri (suala hili linafanyika kwa kushirikisha wawekezajia)
- Kuhamasisha na kuboresha uzalishaji wa zao la chai ili kuendana na malengo yaliyoainishwa kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM,
- Kuboresha miundo mbinu ya barabara kwenye maeneo ya uzalishaji kwa kushirikiana na TARURA na TANROADS,
- Kuendeleza mashirikiano kati ya Taasisi zinazosimamia zao na Kilolo AMCOS, Halmashauri na Ofisi ya Msajili wa Hazina katika ufufuaji wa mashamba na kutafuta ufumbuzi wa suala la ujenzi wa kiwanda cha chai katika Wilaya ya Kilolo;
- Kuendeleza usuluhishi nje ya mahakama kwa wanahisa na wamiliki wa kiwanda cha chai Lupembe.
- Kuhakikisha Wakulima wote wanasajiliwa chini ya vyama vyao katika mfumo wa kielektoniki ili kurahisisha utoaji wa huduma hususan upatikanaji wa mbolea.

# AHSANTE SANA